## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MAELEZO YA SERIKALI KUHUSU UTATUZI WA MGOGORO WA ARDHI KATIKA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA KILIMANJARO

## UTANGULIZI

Katika wiki chache zilizopita kumekuwa na taarifa mbalimbali zisizo sahihi zinazodai kwamba kuna mgogoro wa ardhi katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) baina ya Serikali na wananchi. Ifuatayo ni taarifa rasmi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoelezea ukweli wa suala zima.

## HISTORIA YA ENEO LA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA WA KILIMANJARO (KIA)

Eneo ulipo Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) hivi leo lilianza kumilikiwa na Serikali kabla ya mwaka 1969 na lilijulikana kisheria ***Pori Tengefu la Sanya Lelatema,*** likiwa na eneo la kilomita za mraba **800**.

Wakati huo mwaka 1969 Serikali ilitenga eneo lenye kilomita za mraba 110 (hekta 11,085) kutoka kwenye zile kilomita za mraba 800 kwa ajili ya matumizi ya uwanja wa ndege. Baadaye eneo la KIA lilipimwa rasmi mwaka 1989 kwa ramani ya upimaji Na. **E5255/18** iliyosajiliwa na kupewa Na. **231264**. Eneo lilimilikiwa kihalali kwa hati **Na. 22270.**

Vijiji vilivyopakana na uwanja huu ni Kaloleni, Samaria, Malula na Majengo Kati kwa upande wa wilaya ya Arumeru mkoani Arusha kwa upande wa wilaya ya Hai ni Sanya Stesheni, Tindigani, Chemka na Mtakuja.

Kati ya mwaka 2007 na 2010 wananchi wa jamii ya wafugaji kutoka wilaya ya Arumeru mkoani Arusha na Hai mkoani Kilimanjaro, walianza kuingia, kuweka makazi na kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya eneo la KIA.

Shughuli hizo za kibinadamu zinazohusisha kilimo na ufugaji ndani ya eneo ya uwanja zimekuwa zikiathiri shughuli za uendeshaji hasa katika kipindi cha kiangazi ambapo upepo wa vumbi (kisulisuli) hupelekea uono hafifu kwa marubani kiasi cha ndege kushindwa kutua na hivyo kulazimika kwenda kutua kwa dharura katika viwanja jirani.

Athari nyingine ya shughuli hizo za kibinadamu ni pamoja na kuharibiwa kwa uoto wa asili kwa kukata miti, majani na kulisha mifugo na pia kusababisha Serikali kushindwa kutekeleza mpango wa uwanja huu.

Ili kuhakikisha kunakuwa na uendeshaji salama wa shughuli za uwanja wa ndege ambao unaendana na matakwa na viwango vya kitaifa na kimataifa, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliagiza Serikali itafute fedha kiasi cha shilingi **bilioni 11.3** kwa ajili ya kulipa thamani ya maendelezo yaliyofanywa na wananchi hao kwenye ardhi hiyo ambayo kisheria ni mali ya Serikali. Kiwango hiki kilikuwa ni kwa mujibu wa uthamini wa kitaalam wa mali za wananchi uliofanywa katika eneo hili.

Awali, jumla ya wananchi kutoka kaya **1,712** zilifanyiwa uthamini kwa ajili ya kulipwa gharama za maendelezo waliyofanya katika ardhi ya uwanja huu wa ndege. Zoezi la uthamini lilianza tarehe 17 Novemba, 2022 na kukamilika tarehe 22 Desemba, 2022. Zoezi hili lilijumuisha mali zilizoendelezwa juu ya ardhi pekee, mathalani ujenzi wa makazi au mashamba ya miti ambapo kwa mashamba ya mazao ya muda mfupi wananchi walipewa muda wa kumalizia kuyatunza hadi kuvuna na kuyauza bila budhudha. Uthamini wa ardhi haukufanyika kwa sababu ardhi hii ni mali ya serikali na wananchi waliokuwa wakiishi hapo hawakuwa na umiliki.

Idadi ya wathaminiwa iliyopatikana ilikuwa kaya 1,061 kwa wilaya ya Hai katika vijiji vinne na kaya 651 kwa wilaya ya Arumeru katika vijiji vitatu na kufanya jumla ya kaya 1,712. Sehemu ya ardhi ya vijiji hivi ndiyo iliyokuwa imeingia kwenye eneo la uwanja wa KIA; hivyo uthamini umeathiri ukubwa fulani tu wa sehemu za vijiji hivyo. Mathalani, robo tatu ya kijiji cha Tindigani ndiyo iliyokuwa imeingia uwanjani lakini bado kimebakiza eneo

kubwa liitwalo Bonza ambako watu wengi wamehamia. Aidha, shule ya msingi na zahanati vya Tindigani navyo pia vitahamia Bonza.

Ni vema kufahamisha kwamba wananchi wote waliolipwa wamehamia kwenye vijiji vya jirani au katika maeneo mengine ya vijiji vyao na serikali za vijiji jirani na uwanja wa KIA ziliamua kuwauzia maeneo mapya ya ukubwa wa mita 25 kwa 25 kwa bei ya shilingi 80,000/-. Hakuna wananchi waliobakia bila mahali pa kuishi. Wananchi hao tayari wameshajenga nyumba mpya za kuishi na maisha yanaendelea kwani baadhi yao walianza kujenga hata kabla ya kulipwa na serikali.

Gharama hizo zilihusisha majengo, mazao, posho ya makazi, posho ya usumbufu, posho ya usafiri na fidia ya makaburi. Kimsingi mchanganuo wa malipo upo katika vipengele sita: (i) Majengo; (ii) Mazao ya kudumu; (iii) Posho ya makazi; (iv) Posho ya usafiri; (v) Posho ya usumbufu; (vi) Posho ya makaburi. Kwa ujumla wananchi hadi sasa wameshalipwa jumla ya **shilingi 11,321,898,061.69** ambapo kwa Arumeru ni **shilingi 4,042,854,329.57** na Hai **shilingi 7,279,043,732.12.**

**UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA MALIPO**

Katika utekelezaji wa zoezi la ulipaji, mwezi **Novemba, 2023**, Serikali kupitia uongozi wa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro (ulipo uwanja huu), ulitoa taarifa rasmi kwa wananchi wa kaya 1,712 kupitia mikutano na matangazo ya umma kuhusu hatua za ulipaji na baadaye kutoa notisi kuwataka wananchi hao waondoke kwa hiari yao punde watakapopokea malipo. yao

Mpaka kufikia tarehe 30, **Aprili, 2024,** jumla ya wananchi **1,666** kati ya **1,712** walikwishalipwa malipo yao yenye thamani ya **shilingi bilioni 11.2.** Wananchi hao wameshaondoa maendelezo waliyokuwa wamefanya juu ya ardhi ya KIA na kuhama kwa hiari.

Mpaka kufikia tarehe 14 **Mei, 2024,** ni wananchi **46** tu ndio waliokuwa hawajapokea malipo yao kwa sababu tofauti tofauti zikiwemo kukosa akaunti za benki; kutorfautiana kwa majina yaliyo katika taarifa za malipo na yaliyopo benki; kukosekana kwa uthibitisho wa mirathi kwa wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia; na baadhi ya wananchi kufungua mashauri ya madai mahakama kuu kupinga zoezi la ulipaji linaloendelea.

**TAARIFA KWA WANANCHI**

Serikali ilihakikisha kwamba wananchi wote wanafahamu kila kinachoendelea na kwa suala la tarehe ya kuhama baada ya malipo walipewa siku 21 za kisheria kufanya hivyo mnamo tarehe 10 Machi, 2024, ikianza kuhesabiwa tarehe 11 hadi 31 Machi, 2024. Hata hivyo, waliongezewa siku 19 na kuwa siku 40 hadi Aprili 19, 2024, baada ya Makamu wa Rais kumpa maelekezo Mkuu wa Mkoa. Lakini baada ya hapo waliachiwa muda wa ziada hadi tarehe 7 Mei, 2024, huku wakipewa matangazo na hata kuwafuata mmoja mmoja wenye changamoto.

Aidha, Kamati ya Usalama ya Wilaya nayo ilipita kwenye serikali za vijiji na kuhakikisha inawataarifu wananchi kwamba muda wa kuondoka sasa umefika. Hata hivyo, ilipofika tarehe 7 Mei, 2024, kilichofanyika ilikuwa kubomoa makazi ambayo wamiliki walikuwa wameshaondoka na kwa wale waliosahau mali zao walitafutwa na kurejeshewa. Hili lilikuwa ni zoezi la kuondoa mapagale na mabaki na si kuvunja makazi.

Serikali inaendelea kutatua changamoto hizo kwa kuhakikisha nyaraka za uthibitisho wa mirathi; viapo vya majina na vitambulisho vya taifa vinapatikana kwa wananchi ambao hawakuwa navyo. Aidha, mashauri ya madai yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali yameondolewa mahakamani; hivyo hakuna zuio la utekelezaji wa zoezi la malipo.

Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwezi **Juni 2024** kila mwananchi awe amechukua malipo yake. Ni vyema ikaeleweka wazi kwamba, wananchi ambao hawajachukua malipo bado wapo kwenye makazi yao ndani ya eneo la KIA.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI BAADA YA WANANCHI KUONDOKA NDANI YA ENEO LA UWANJA WA NDEGE**

Ili kuondoa shughuli za kibinadamu ndani ya eneo la KIA, na kuongeza kiwango cha ulinzi na usalama wa 6uwanja na miundombinu yake na kuongeza ufanisi katika uendeshaji na uendelezaji wa uwanja, Serikali baada ya wananchi kuondoka kwa hiari katika eneo la uwanja inafanya yafuatayo:

i. Kuchonga barabara ya mzunguko (peripheral road) kuzunguka eneo lote la mpaka wa uwanja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama;
ii. Kuweka alama kubwa (beacons) za kudumu ambazo zinaonekana kwa urahisi kuzunguka uwanja kwa ajili ya kulinda mipaka;

    **IKUMBUKWE** kwamba kazi hii ilianza tarehe 17 Novemba, 2022 ma kukamilika Desemba 2022. Jumla ya alama 186 za nguzo fupi za zege ziliweka katika mzingo wa km 53. Uzinduzi wa zoezi hili ulifanywa kwa uwazi ambapo Mkuu wa Mkoa, Mhe. Nurdin Babu, ndiye aliyezindua.

iii. Kuondoa na kusafisha mapagale yaliyoachwa na wananchi walioondoka kwa lengo la kuweka mazingira ya uwanja katika hali safi na salama;
iv. Kuanza kurejesha uoto wa asili ndani ya eneo husika; na
v. Kuendelea kufanya mikutano ya ujirani mwema kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu ulinzi na usalama wa maeneo ya viwanja ndege kwa maendeleo endelevu ya taifa.

**HITIMISHO**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, inapenda kuuhakikishia umma kuwa, itaendelea kulinda na kusimamia misingi ya haki za binadamu na utawala bora katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiserikali.

Aidha, Serikali inatambua mchango wa jamii ya wakulima na wafugaji, katika uchumi wa nchi pamoja na ushiriki wao katika kuulinda na kuutunza uwanja huu wa kimataifa ambao ni lango muhimu la watalii wanaokuja nchini mwetu.

Serikali inatoa rai kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya viwanja ya ndege vyote hapa nchini, kushiriki kikamilifu katika kutunza na kulinda ardhi za viwanja hivyo vya ndege ili viendelee kutoa huduma zinazoendana na viwango vya kitaifa na kimataifa. Kwa wananchi ambao hawajachukua malipo yao, wanaombwa kushughulikia vikwazo walivyo navyo ili waweze kuchukua malipo yao.

*Maelezo.*